



# Karibu Chekechea!



2022-23

**Chekechea imeonyesha kuwa inaweka njia ya mafanikio katika masomo!**

Wazazi wamekuwa na maswali kuhusu kufaulu na masomo wakati wanafunzi wanapitia kila darasa. Mwongozo huu utakuelekeza na kujibu maswali katika kumsaidia mwanafunzi wako kufikia kumaliza shule.

Mtoto wangu  
anajifunza nini?

Viwango vinaelezwa na jimbo la Oregon kuwa mwanafunzi anatakiwa kujua na ajue kufikia mwisho wa mwaka wa shule.

## Kujua kusoma na kuandika

Sifa za wasomaji wa Chekechea:

- Kuonyesha kupenda vitabu
- Anajibu maneno yaliochapiswa
- Anajua sauti na herufi
- Anaanza kuweka mikakati katika kusoma
- Anaendeleza mkakati katika kusoma



Angalia sampuli ya Chekechea kusoma & kuandika katika kiwango cha darasa

## Msingi wa hesabu

Sifa za wasomaji Chekechea katika Hesabu:

- Kujua namba na kuhesabu mpaka 20
- Kuhesabu na kujua idadi ya vitu
- Kulinganisha namba
- Kujumuisha kutoa na kujumlisha namba ndani ya 10
- Kucheza na namba 11-19 ili kujenga msingi wa namba
- Kutenganisha, kujenga, kuelezea na kulinganisha vitu



Angalia sampuli ya Chekechea hesabu katika ngazi ya darasa

Ni nini kinatakiwa  
ili kuweza  
kuhitimu?

**Unaweza kuona ajabu kuanza kufikiria kuhusu kumaliza high skuli wakati mtoto wako yuko shule ya msingi. Lakini ni muhimu kuanza kuweka malengo mapema.**

Shule za msingi ni wakati ambao mwanafunzi anaweka msingi na maarifa ambao anajenga kila baada ya mwaka.

Njia muafaka ni kumuwekea mwanafunzi wako malengo na kuhitimu shule kwa kuyafikia kila mwaka. Sasa ndiyo wakati wa kuanza.

Mtoto wangu  
anaendeleaje?

Kushiriki katika elimu ya mtoto wako ni muhimu.

Kwa wanafunzi wengi, kuona wazazi hao wanafuata masomo yao inawasaidia kuwaweka katika njia ya kumaliza shule.

Hii ni njia mojawapo kuwashirikisha wazazi wajue mtoto/watoto wanavyofanya darasani na kuwapatia msaada unaotakiwa ili waweze kufanikiwa.



## Ripoti ya maendeleo

Wazazi wa wanafunzi kwa shule za msingi wanapokea taarifa ya maendeleo mara tatu (ripoti tatu) kila mwaka. Shule za msingi za Salem-Keizer wanatumia mfumo wa ustadi kwenye kusahihisha maana alama zinaonyesha uelewa wa mwanafunzi kuelekea kusimamia kujua.

Alama zimeandikwa kwa kufuata uzito ndani ya 1 mpaka 4 kwa maana alama hizi zinaonyesha maendeleo katika kuelewa pia kufikia viwango vya darasa. Alama 3 inaonyesha mwanafunzi amefikia kiwango cha darasa na anamendeleo mazuri.



## Ongea na mwalimu wa mwanafunzi

Maongezi na mwalimu ni njia pekee kujua maendeleo ya mwanafunzi. Email/barua pepe au kupitia app ya ParentSquare ni njia ya haraka zaidi kuweza kuwasiliana na mwalimu. Pia walimu wanaweza kupatikana kwa njia ya simu baada ya muda wa darasa.

Kumbuka ni muhimu kuhudhuria mikutano ya wazazi na walimu! Tafadhali tumia hii nafasi kupata kuonana na mwalimu wewe mwenyewe.



## Tathmini inayoendelea

Kuanzia chekechea mpaka darasa la pili, mwalimu anaendelea kuangalia kazi ya mwanafunzi kama inakwenda sawa na kiwango cha maendeleo. Hii inaitwa "tathimi inayoendelea"

Wanafunzi wakubwa (darasa 3-8 na 11) wanafanya mitihani ya Jimbo kila mwaka kwenye kusoma, kuandika na hesabu. Darasa 5, 8 & 11 pia wanafanya mitihani wa sayansi kila mwaka. (Hii mitihani inasaidia Idara ya Elimu ya Oregon kujua kama shule zinasaidia wanafunzi kufikia viwango vinavyotakiwa)

Walimu katika haya madarasa ya juu wanatumia mitihani kama taarifa kufanya tathmini inayoendelea na vipimo kusaidia wanafunzi kujifunza. Huko baadaye wazazi pia wanaweza kutumia hii mitihani kama njia ya kujua wanafunzi wao wanafanyaje mashuleni.

Nitawezaje  
kumsaidia  
nyumbani?

Kama mzazi au mlezi una nafasi kubwa katika kushawishi mafanikio ya baadaye kwa mtoto wako.

Kuna mambo mengi unaweza kufanya ili kuweka msingi wa mafanikio ya mtoto wako shuleni kutoka nyumbani.

## Njia ya kumsaidia mtoto wako kumaliza shule nyumbani

- Onyesha mtazamo mzuri kuhusu shule na mtoto wako atafuata mtazamo huo.
- Jua kuhusu dhana ya kitaaluma kwa mtoto wako ni kujifunza (kugeuza upande)
- Tengeneza mahali pazuri kwa ajili ya kufanya kazi ya shule na kupunguza fujo au vurugu (Zima TV na michezo ya video)
- Hakikisha kuna vifaa vya shule kama karatasi na penseli. Wasiliana na shule kama unahitaji msaada.
- Soma vitabu vya kutunga na mwanafunzi wako na muongee yaliyotokea kwenye kitabu
- Mkazanie kuandika nyumbani. Muandikie pamoja kwa kuelezea kiundani.
- Ongea na mtoto wako kuhusu kazi mbalimbali wanazozifanya watu na ujuzi unaotakiwa
- Mwambie mtoto wako afanye hesabu rahisi kila siku mpaka ajue kugeuza namba na mpagingilio tofauti
- Jitahidi uwezavyo kumsaidia mtoto wako kuwa na mahudhuro na ushiriki darasani. Mahudhuri ya ushiriki shuleni ni muhimu haswa kwa wale wachanga kwenye kujifunza. Tumia ParentVUE kuangalia mahudhuri na kumhamasisha kushiriki shughuli za darasani na kila siku
- Angalia app ya ParentSquare mara kwa mara na uwe na maongezi ya wazi kwenye shule ya mtoto wako.